**HOTUBA YA KATIBU MTENDAJI WA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA NDG. GEORGE NATHANIEL MANDEPO WAKATI WA UFUNGUZI WA MAFUNZO KUHUSU MIFUMO YA SHERIA ZA NISHATI NA MFUMO WA SHERIA ZA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI NCHINI TANZANIA YALIYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA APC – BUNJU - DAR ES SALAAM, TAREHE 18/ JUNI 2026.**

**Bw.Josiah Mwabeza: Mwakilishi wa** Tume ya Taifa ya Mipango;

**Menejimenti ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania;**

**Wawezeshaji wa Mafunzo wote mliopo;**

**Washiriki wote wa Mafunzo kutoka**: Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Tume ya Taifa ya Mipango, na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania! …………………………!!**

**Kazi na Utu! ……………………………………………………!!**

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji, Washiriki**,

Awali ya yote, napenda kuchukua wasaa huu kushukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye ametujalia uzima na afya na kutukusanya hapa siku ya leo katika ufunguzi wa mafunzo haya muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu.

Tunaendelea kumpongeza na kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt, Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makuu ya kuwezesha Taifa kuwa na Dira mpya ya Maendeleo 2050. Kwa ajili ya hilo, leo hii tumekutana hapa ili kuweza kushiriki kikamilifu ikiwa ni mpango mmoja wapo wa utekelezaji wa Malengo ya Dira hiyo yenye manufaa kwa Taifa hata mwaka 20250.

Nashukuru sana pia Uongozi mzima wa Wizara ya Katiba na Sheria,Wizara ya Fedha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Mipango, Mwandishi Mkuu wa Sheria na wadau wote ambao wamewezesha kazi hii kufanyika.

Napenda kuchukua fursa hii pia kukukaribisheni nyote kwa dhati kabisa katika mafunzo haya muhimu. Ninakushukuru sana kwa kuitikia wito wetu. Uwepo wenu hapa leo, mkiwa mmetoka katika sekta mbalimbali za kimkakati, ni uthibitisho tosha wa umuhimu mkubwa wa mafunzo haya kwa siku zote mbili za mafunzo haya.

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji, Washiriki**,

Kama mnavyofahamu, tarehe 17 Julai, 2025, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (*Dira 2050*), aliielekeza Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya maboresho ya Sheria ili kuwezesha Utekelezaji kamili wa Dira 2050.

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji, na Washiriki wa Mafunzo,**

Katika kutekeleza maagizo hayo ya Mheshimiwa Rais,Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wadau wa Kundi Na. 4 ambao ni Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Tume ya Taifa ya Mipango, na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria imefanya Uchambuzi **wa Mifumo 28** itakayofanyiwa maboresho katika kipindi cha miaka mitatu - 2026/2027 hadi 2028/2029. Mifumo hiyo ni pamoja na: Mfumo wa Sheria za Nishati, Mfumo wa Sheria za Viwanda, Biashara na Uwekezaji, ambapo mapitio ya mifumo hiyo ya Sheria itaanza mapema mwezi Julai, 2026.

## MUHIMU WA KUBORESHA SHERIA KWA AJILI YA DIRA 2050

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji na Washiriki wa Mafunzo,**

Maboresho ya sheria ni nguzo mama katika kuweka mazingira wezeshi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yatakayoruhusu utekelezaji wenye tija na ufanisi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Ili nchi iweze kufikia malengo yake ya muda mrefu, ni lazima mfumo wa sheria uendane na mabadiliko ya kiteknolojia, kiuchumi na kijamii ya karne ya 21.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inalenga kuijenga Tanzania kuwa nchi yenye uchumi shindani, jumuishi, unaotegemea maarifa, ubunifu, teknolojia na uzalishaji wenye tija. Hivyo, mifumo ya sheria inayotawala sekta za nishati, viwanda, biashara na uwekezaji lazima iwe kichocheo cha maendeleo badala ya kuwa kikwazo cha maendeleo.

Maboresho ya sheria yatasaidia:

- Kuondoa sheria zisizoendana na wakati na zinazokwamisha ubunifu, biashara na uwekezaji.
- Kurasimisha na kurahisisha michakato ya kiutendaji katika sekta za umma na binafsi.
- Kukuza utawala bora, uwajibikaji, haki na usawa kama msingi wa maendeleo endelevu.
- Kuimarisha ushindani wa Tanzania katika kuvutia uwekezaji wa ndani na wa kimataifa.
- Kuweka mazingira bora ya ukuaji wa uchumi wa viwanda, biashara na uchumi wa kidijitali.

Ndugu Washiriki,

Katika karne ya 21, maendeleo ya teknolojia yamebadili kwa kiasi kikubwa namna biashara, uwekezaji na utoaji wa huduma unavyofanyika duniani. Kwa sababu hiyo, mapitio ya sheria zetu yanapaswa kuangalia kwa kina maeneo ya biashara za kidijitali, matumizi ya akili mnemba (Artificial Intelligence), usalama wa taarifa, mifumo ya kidijitali ya utoaji huduma, na mifumo ya kisasa ya uwekezaji.

Ni muhimu kuhakikisha kuwa sheria zetu zinaendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia ili Tanzania isiwe mtazamaji wa mabadiliko ya dunia bali mshiriki na mnufaika wa mabadiliko hayo.

Ndugu Viongozi, Wawezeshaji na Washiriki,

Katika zoezi hili la maboresho tumeandaa Ramani ya Utekelezaji (Road Map) inayonyesha Mifumo ya Sheria 28. Tumeanza na Sheria za Nishati, Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Tunapozungumzia sheria za nishati, ni lazima tukumbuke kuwa hakuna maendeleo ya viwanda bila uwepo wa nishati ya uhakika. Nishati ndiyo

injini ya maendeleo ya viwanda, biashara, uwekezaji, huduma za kijamii na uchumi wa kidijitali.

Hivyo, maboresho ya sheria za nishati yanapaswa kuzingatia upatikanaji wa nishati nafuu, salama, endelevu na rafiki kwa mazingira. Aidha, ni muhimu kuendelea kujenga mazingira yatakayowezesha ushiriki wa sekta binafsi kupitia mifumo mbalimbali ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP) kwa manufaa ya taifa.

Katika mazingira ya ushindani wa kimataifa, nchi zinazofanikiwa kuvutia uwekezaji ni zile zenye sheria zinazotabirika, zilizo wazi, zinazotekelezeka kwa urahisi na zinazotoa uhakika kwa wawekezaji.

Tanzania inapaswa kuendelea kujijengea sifa ya kuwa kituo bora cha biashara na uwekezaji katika Afrika Mashariki na Bara la Afrika kwa ujumla. Hili haliwezi kufikiwa bila kuwa na mifumo madhubuti ya sheria inayojibu mahitaji ya sasa na ya baadaye.

Sheria za Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni nyenzo muhimu katika kuwezesha Uchumi jumuishi

## WITO WA MAGEUZI YA KISHERIA KWA TANZANIA YA 2050

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji na Washiriki wa Mafunzo,**

Tunapoelekea mwaka 2050, tunapaswa kutambua kuwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia, biashara, uwekezaji, mazingira na mahusiano ya kimataifa inaongezeka kwa kiwango kikubwa sana.

Hali hii inahitaji mifumo ya sheria inayoweza kujibu changamoto za sasa na za baadaye. Wajibu wetu si kurekebisha sheria kwa ajili ya leo pekee, bali kujenga mfumo wa sheria utakaoihudumia Tanzania kwa miongo mingi ijayo.

Tunapaswa kuwa na sheria zinazochochea ubunifu, zinazoimarisha ushindani wa kiuchumi, zinazoendeleza matumizi ya teknolojia, zinazoimarisha uwekezaji na zinazolinda maslahi mapana ya taifa katika mazingira ya utandawazi.

Mwisho wa yote, maboresho ya sheria tunayoyajadili hapa leo si kwa ajili ya taasisi pekee, bali kwa manufaa ya mwananchi wa kawaida. Tunataka

kuona sheria zinazochochea ajira kwa vijana, zinazoimarisha mazingira ya biashara kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati, zinazovutia uwekezaji wenye manufaa kwa wananchi, na zinazoboresha maisha ya Watanzania wote.

Mafanikio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 hayatategemea tu uwepo wa sera bora, bali pia uwepo wa sheria bora, taasisi imara, na wataalamu wenye maono ya muda mrefu.

Kama alivyosisitiza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa uzinduzi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, maendeleo ya taifa letu yanahitaji mifumo imara ya sheria inayoweza kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya dunia.

Sheria bora si mkusanyiko wa vifungu pekee; ni nyenzo ya maendeleo, haki, uwekezaji, ubunifu na ustawi wa wananchi. Tanzania ya mwaka 2050 tunayoitamani itajengwa si kwa rasilimali tulizonazo pekee, bali pia kwa uwezo wetu wa kuwa na mfumo wa sheria unaotabirika, unaotekelezeka na unaoendana na wakati.

Kwa ufupi, maboresho haya yatasaidia:

- Kuondoa sheria zilizopitwa na wakati zinazokwamisha ubunifu na uwekezaji.

- Kurasimisha na kurahisisha michakato ya kiutendaji serikalini na kwenye sekta binafsi.

- Kuhakikisha uwepo wa utawala wa sheria, haki na usawa kama msingi wa maendeleo endelevu.

## UTEKELEZAJI WA AGIZO

Ikiwa ni utekelezaji wa Maelekezo ya Serikali yalitolewa wakati wa kuzindua Dira, kwa kushirikiana na wadau wa Taasisi za Maboresho ya Sheria, tumeandaa Andiko la Programu ya Maboresho ya Sheria pamoja na Ramani ya Utekelezaji (Road Map) kwa kipindi cha miaka mitano 2026/2027 hadi 2030/2031 ili kuwezesha Utekelezaji Kamili wa Dira 2050.

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji, na Washiriki wa Mafunzo,**

Kwa kuzingatia umuhimu na Watafiti kuwa na uelewa wa kina kuhusu mifumo ya Sheria tajwa hapo juu itakayofanyiwa tafiti na mapitio, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania pamoja na wadau wa Kundi Na. 4 kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango imeandaa mafunzo kuhusu **Mfumo wa Sheria za Nishati na Mfumo wa Sheria za Viwanda, Biashara, na Uwekezaji** kwa washiriki ambao watashiriki katika kufanya tafiti na mapitio ya Sheria hizo.

Mafunzo haya yanalenga kujenga uelewa wa pamoja, kubadilishana uzoefu, na kuweka mikakati thabiti ya kufanya tafiti na kufanya mapitio ya **Sheria za Nishati**, **Viwanda, Biashara, na Uwekezaji** nchini Tanzania ili kuzifanya ziendane na Dira 2050 kama maelekezo ya Mhe. Rais yalivyoelekeza.

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji, na Washiriki wa Mafunzo,**

Tanzania imepiga hatua kubwa sana katika mageuzi ya sekta ya nishati na uwekezaji. Miradi mikubwa kama Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), uwekezaji katika nishati ya gesi asilia, na miradi ya nishati jadidifu (*renewable energy*) ni mifano dhahiri ya mwelekeo wa nchi yetu.

Hata hivyo, mafanikio ya miradi hii yanategemea sana jinsi sheria zetu za nishati na uwekezaji zinavyoendana na wakati. Mathalan, lazima tujiulize: Je, sheria zetu za nishati zinajibu changamoto za sasa za mabadiliko ya tabianchi? Je, sheria zetu za usambazaji wa nishati zinatoa fursa sawa kwa sekta binafsi kushirikiana na Serikali kupitia mifumo ya PPP (*Public-Private Partnership*)? Je, Sheria zetu za nishati zinatoa fursa ya kuwa na gharama nafuu ya huduma kama umeme kwa wanachi? Je, Sheria zetu za nishati zinachochea matumizi ya nishati safi?

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,**

Wakati tukiziangazia sheria za nishati, ni muhimu pia tuangalie pia Sheria za Viwanda, Biashara, na Uwekezaji. Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania (Tanzania Investment Act) na Sheria nyingine katika sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Sheria hizi zote zimefanyiwa maboresho mara kadhaa lakini bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali. Hivyo, ni muhimu sheria hizo zikafanyiwa Mapitio na Utafiti wa Kina ili ziendane na matarajio ya Dira 2050.

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji, na Washiriki wa Mafunzo,**

Washiriki wote mliopo hapa, mnao wajibu mkubwa wa kuhakikisha Sheria katika sekta za Nishati, Viwanda, Biashara na Uwekezaji zinaboreshwa ili kuwezesha utekelezaji kamili wa Dira 2050 na maendeleo yaliyokusudiwa katika sekta hizi. Ni muhimu kufahamika kuwa maboresho husika ya sheria yatahusisha Mapitio na Utafiti wa kina ili kuona na kujiridhisha jinsi Sheria husika zinavyochochea au kukwamisha Utekelezaji kamili wa Dira 2050.

Natambua pia kuwa mkusanyiko huu unahusisha wataalamu wa kada zingine na wenye uzoefu tofauti tofauti katika Sekta tunazofanyia kazi, hivyo ushirikiano wa pamoja katika kazi hii ni muhimu katika kuhakikisha kuwa sheria zitakazofanyiwa utafiti, mapitio na ambazo pia zitatungiwa sheria baada ya michakato hii kukamilika zinaendana na Mipango ya kitaifa na Dira 2050.

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji, na Washiriki wa Mafunzo,**

Niwaombe sana washiriki muwe na mafunzo ya kujenga na mijadala yenye uwazi. Jadilini changamoto zilizopo hususan urasimu wa kisheria unaochelewesha uwekezaji nchini kwetu. Toeni mapendekezo ya jinsi ya kurahisisha usajili wa biashara, uwekezaji, utatuzi wa migogoro ya kibiashara kupitia usuluhishi (*arbitration*), na jinsi ya kulinda rasilimali za nchi yetu bila kuwa na mawazo yanayotishia uwekezaji na wawekezaji wanaokuja kuwekeza hapa nchini kwetu. Tuweke umakini mkubwa pia katika kuchambua na kuzijua vizuri Sheria za Nishati na Viwanda zilizopo. Maeneo hayo ya kisekta ni nguzo muhimu katika kufikia malengo ya Serikali.

## HATUA ZINAZOTARAJIWA KUCHUKULIWA KATIKA MABORESHO YA SHERIA

Utekelezaji wa maboresho ya Sheria utazingatia misingi ya **Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria (Sura ya 171)** pamoja na **Kanuni za Mapitio na Tathmini**, ambapo hatua zifuatazo zitachukuliwa:

- **Ufanyaji wa Mapitio ya Kina (Comprehensive Law Review):** Kwa uratibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Serikali itafanya utafiti na mapitio ya sheria zote za kisekta ili kubaini maeneo yanayokinzana au yanayokwamisha malengo ya Dira 2050.

- **Ushirikishwaji wa Wadau (Stakeholder Engagement):** Kukusanya maoni **kutoka** sekta binafsi, asasi za kiraia, wataalamu wa sheria na

wananchi kwa ujumla ili kuwa na sheria zinazokidhi mahitaji halisi ya jamii.

- **Ulinganifu wa Sheria na Mifumo ya Kikanda/Kimataifa (Harmonization):** Kuhakikisha sheria za ndani zinawiana na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo nchi imeridhia ili kukuza biashara na ushirikiano wa kimataifa.

- **Uandishi wa Sheria kwa Lugha Rahisi na Sahihi:** Kurekebisha rasimu za sheria ili ziweze kueleweka kwa urahisi na **watekelezaji** pamoja na wananchi wa kawaida, hivyo kupunguza migogoro ya kisheria.

## MATOKEO TARAJIWA YA MABORESHO YA SHERIA

Baada ya kukamilika kwa hatua za maboresho, matokeo yafuatayo yanatarajiwa kuonekana kuelekea mwaka 2050:

I. **Ongezeko la Tija na Ufanisi wa Taasisi za Umma:** Sheria mpya zitapunguza urasimu usio wa lazima na kuongeza uwajibikaji na kasi ya utoaji wa huduma kwa jamii.

II. **Mazingira Bora na Salama ya Uwekezaji:** Uwepo wa sheria madhubuti na za kisasa utavutia mitaji ya ndani na nje, na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda na kidijitali.

III. **Kuimarika kwa Upatikanaji wa Haki:** Kupitia kanuni bora za mapitio na tathmini, mifumo ya utoaji haki itakuwa ya haraka, ya gharama nafuu na yenye usawa kwa wote.

IV. **Sheria Zinazoishi na Wakati (Dynamic Legal Framework):** Kuwepo kwa mfumo endelevu wa kutathmini sheria ili **kuhakikisha** hazipitwi na wakati hata mazingira ya nchi yanapobadilika kuelekea 2050.

Ninaamini kuwa maarifa yatakayopatikana katika mafunzo haya yatakuwa msingi muhimu wa kufanya mapitio ya sheria kwa kina, kuandaa mapendekezo yatakayosaidia Serikali, na hatimaye kuweka mfumo wa sheria utakaowezesha Tanzania kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

## HITIMISHO

**Ndugu Viongozi, Wawezeshaji, na Washiriki,**

Kabla sijahitimisha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, Tume ya Taifa ya Mipango, na wawezeshaji wetu wote ambao wamefanya kazi usiku na mchana kuhakikisha mafunzo haya yanafanyika katika mazingira haya mazuri na tulivu.

Ndugu Viongozi, Wawezeshaji na Washiriki, jukumu lililo mbele yetu ni kubwa, lakini uwezo wa kulitekeleza upo.

Historia inaonyesha kuwa mataifa makubwa hayakujengwa kwa rasilimali pekee, bali kwa taasisi imara na sheria bora. Tanzania ya mwaka 2050 itajengwa kwa msingi huo huo.

Kupitia ushirikiano wetu, weledi wetu na uzalendo wetu, tunaweza kujenga mfumo wa sheria utakaowezesha Tanzania kuwa taifa lenye uchumi shindani, lenye viwanda imara, lenye uwekezaji wenye tija na lenye ustawi kwa wananchi wake wote kuelekea mwaka 2050.

Ninaamini kuwa maarifa, uzoefu na mapendekezo yatakayozaliwa kupitia mafunzo haya yatakuwa msingi muhimu wa mageuzi ya sheria yatakayoiwezesha Tanzania kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Kila mchango utakaotolewa hapa ni uwekezaji katika mustakabali wa taifa letu na vizazi vijavyo.

Baada ya kusema hayo, sasa nina furaha na heshima kubwa kutangaza rasmi kuwa Mafunzo kuhusu Mifumo ya Sheria za Nishati, Viwanda, Biashara na Uwekezaji nchini Tanzania yamefunguliwa rasmi.

MUNGU IBARIKI TANZANIA

MUNGU ZIBARIKI TAASISI ZETU

MUNGU AIBARIKI KAZI HII YA MABORESHO YA SHERIA

Asanteni sana kwa kunisikiliza.